بسم الله الرحمن الرحيم

**Kauli zilizotolewa na Waziri Mkuu Nawaf Salam kuhusu Hamu yake ya Kuhalalishwa Haraka kwa Mahusiano na Mayahudi Haziwawakilishi Waislamu kwa vyovyote vile!**
**Badala yake, zinamwakilisha yeye na wale waliomleta madarakani. Kauli hizi ni khiyana kwa Mwenyezi Mungu, Mtume wake na Waumini!**
**(Imetafsiriwa)**

Katikati ya angahewa Amerika inaenea katika eneo hili kupitia kwa rais wake Trump, akitoa wito wa amani na Mayahudi, na kwa mujibu wa Makubaliano ya Abraham yaliyokuja wakati wa ziara yake ya kuchukiza katika eneo hilo, na kujisalimisha kwa watawala wa Kiarabu na Waislamu kwenda sambamba na ajenda hii, hadi kufikia kiwango ambacho mbora zaidi kati yao anaweza kusema ni "tutakuwa wa mwisho kuhalalisha mahusiano na Mayahudi", katika muktadha huu wa Mahojiano Waziri Mkuu wa Lebanon Nawaf Salam wakati wa mahojiano na Mtandao wa CNN, yaliyochapishwa mnamo 30/5/2025, ambapo alisema: "Uhalalishaji mahusiano ni sehemu muhimu ya amani tunayotaka kuona kesho, sio kesho kutwa!"

Alipoulizwa kuhusu njia tofauti ya mazungumzo na uhusiano wao, jibu lake lilikuwa kwamba hapendi wazo la njia mingi. Hii inaashiria anataka kuchukua hatua za haraka kuelekea kujisalimisha kwa Mayahudi, hata bila ya kufungamana na mchakato wa amani wa Palestina! Lakini kauli hizi zilizua kukataliwa na mabishano makubwa, hali iliyopelekea afisi yake ya vyombo vya habari kutoa tamko la kuwataka watu kutazama mahojiano kamili na sio kuyatoa nje ya muktadha au kuyaweka katika mifumo ya uongo. Ilisema kwamba misimamo ya Salam iko dhahiri na haijaachwa wazi kufasiriwa au kupotoshwa, na kwamba "Lebanon inafuata misimamo ya Waarabu, na kwamba uhalalishaji wowote wa mahusiano na Israel unaweza kuja tu baada ya kuasisiwa kwa dola ya Palestina, sio tu kupitia makubaliano juu ya njia," na kwamba "amani inayokubalika na Israel ni amani ya haki na ya kina iliyojengwa juu ya Mpango wa Amani wa Kiarabu ulioidhinishwa jijini Beirut."

Iwe msimamo wake ni kuharakisha uhalalishaji mahusiano bila kuufungamanisha na njia ya amani, au kuambatana na misimamo ya Waarabu ya kusalimu amri, misimamo yote miwili ni upuuzi na haina thamani kwa Waislamu.

Kunukuu Mpango wa Amani ya Waarabu au kuanzishwa kwa dola ya Palestina, ambayo ni, kuomba usaliti wa pamoja au kujisalimisha kwa wale wanaodai kuwawakilisha watu wa Palestina, hakuhalalishi matamshi haya au haraka hii ya uhalalishaji mahusiano. Kadhia ya Palestina si kadhia ya Waarabu kwa misingi ya ukabila, wala si kadhia ya Palestina yenye msingi wa utaifa. Bali ni kadhia ya Uislamu na watu wake ndio sababu ya watu wema kumwaga damu zao ili ardhi hizi ziwe ngome za heshima kwa Uislamu na Waislamu. Wanaendelea kutoa maisha yao kwa ajili ya kuwaondoa Mayahudi wanyakuzi, wanaokalia kimabavu kutoka katika ardhi za Waislamu.

Kwa hiyo, kauli kama hizo zinawakilisha wale tu waliozitoa, si Waislamu. Kwa kweli, wanawakilisha wale waliomwingiza madarakani. Ama msimamo wa Waislamu nchini Lebanon, ni msimamo wa ummah, sio wa dola fulani hapa au pale.

La ajabu juu ya kauli kama hizi ni kwamba zinakuja huku maadui wa Mwenyezi Mungu na Waislamu, Mayahudi wangali wanamwaga damu za watu wetu wa Palestina kwa jumla na hasa Gaza, wakiweka aina kali zaidi za mzingiro, uharibifu, njaa, mauaji, na kufanya kazi ya kulazimisha watu kuyahama makaazi yao mbele ya ulimwengu mzima! Zaidi ya hayo, ndege na droni za Kiyahudi zimekuwa zikizunguka anga za nchi hii ambayo yeye ndiye Waziri Mkuu kwa zaidi ya mwaka mmoja, zikifanya mauaji na uharibifu bila kujali hata kidogo kile wanachokiita ubwana au uhuru. Hawajali mikataba ya kusitisha mapigano, shutuma za kimataifa, au dhamana za Marekani!

Amerika hii hii inaona kwamba kukuweka chini ya mashambulizi ya Kiyahudi na mashambulizi ya mara kwa mara ndiyo mazingira yanayofaa zaidi kwako kuwasilisha na kujisalimisha kwa mradi wake wa kieneo. Na tusisahau kwamba Nawaf Salam alikuwa jaji katika Mahakama ya Kimataifa ya Uadilifu kabla ya kuwa Waziri Mkuu, nafasi ambayo ilipaswa kuwawajibisha wahalifu wa Kiyahudi kwa makosa yao dhidi ya binadamu, si kufanya nao amani!

**Ewe Waziri Mkuu,** ni msukumo gani huu unaoonyesha katika kutafuta amani na uhalalishaji mahusiano na Mayahudi, kutaka iwe kesho na si kesho kutwa?! Hii inaashiria kwamba umechukua hatua nyingi katika kujisalimisha kwa Mayahudi hadi kwamba jambo hilo haliko tena chini ya meza kwa ajili ya aibu mbele ya Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, na waumini, bali limetangazwa waziwazi mezani kwa kauli zisizo na utata, zilizotupwa kwenye nyuso za Waislamu wa Lebanon ili wakubali kuwatayarisha kuwaona Mayahudi wanyakuzi, wanaokalia kwa mabavu wanaozunguka nchi nzima, wakati huu kama watalii, na sio wavamizi!

Haya yote yanafichua zama hizi mpya kuwa ni za uhalalishaji mahusiano na Mayahudi na kuwafungulia nchi kwa kisingizio cha kujikita katika kuleta mageuzi na kuiendeleza Lebanon!

**Ewe Waziri Mkuu,** neno la mwisho kwako na kwa wale wanaofuata au watakaofuata njia hii: Lebanon, kama Palestina, ni sehemu ya ardhi ya Uislamu na haikubali mgawanyiko kwa njia yoyote ile. Bali, itabakia kuwa na umoja dhidi ya miradi hii ya khiyana, bila kujali ni kiasi gani unafikiri au inaonekana kwamba unafanikiwa katika juhudi zako za kuficha sababu za Waislamu. Sauti yetu itabaki kuwa kubwa masikioni mwako ikisema kile ambacho wewe na wafuasi wako mnachukia mpaka Mwenyezi Mungu atakapotimiza hukmu yake kwa kuwahuisha Waislamu na kusimamisha dola yao: Dola ya pili ya Khilafah kwa njia ya Utume. Dola isiyofanya mapatano na Mayahudi wala kuafikiana nao, bali inasambaratisha kila ulichotia sahihi au utakachotia saini, na kupigana nao kwa kutimiza ahadi ya Mola wetu Mlezi:

[فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ لِيَسُوءُوا وُجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا الْمَسْجِدَ كَمَا دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبِّرُوا مَا عَلَوْا تَتْبِيراً]

**“Na ikifika ahadi ya mwisho ili waziharibu nyuso zenu, na waingie Msikitini kama walivyo ingia mara ya kwanza, na waharibu kila walicho kiteka kwa uharibifu mkubwa.”** [Surat Al-Isra:7]. Na katika bishara njema kutoka kwa Mtume wetu Muhammad (saw): **«تُقَاتِلُكُمْ يَهُودُ فَتُسَلَّطُونَ عَلَيْهِمْ، حَتَّى يَقُولَ الْحَجَرُ: يَا مُسْلِمُ، هَذَا يَهُودِيٌّ وَرَائِي فَاقْتُلْهُ» “Mtapigana na Mayahudi. Mtapata udhibiti juu yao, mpaka jabali litasema: Ewe Muislamu! Yahudi huyu yuko nyuma yangu basi muue!”**

Hii ndiyo imani ya Waislamu wanaoishi miongoni mwao kupitia Qur’an na Sunnah, na hivi ndivyo watoto wa Waislamu wanavyolelewa kuwaona Mayahudi kuwa ni wauaji wa manabii na mitume, wanyakuzi wakaliaji kimabavu, na wauaji wa ndugu zao na Waislamu wenzao nchini Palestina. Haijalishi ni kauli gani utakazotoa au makubaliano gani unayotia saini chini ya lebo yoyote, imani hii haitabadilika.

**Ama nyinyi Waislamu nchini Lebanon:** misimamo yenu leo lazima itangazwe na kudhihirika kutoka kwenye mimbari zenu, katika misimamo yenu na kauli zenu zote, na katika kila uwanja na mkusanyiko ili msije mkaingia katika dhambi ya kauli hizi ikiwa mtasitasita au kupitisha sehemu yoyote ya uovu huu. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt) kama ilivyosimuliwa na Abu Dawud:

**«إِذَا عُمِلَتْ الْخَطِيئَةُ فِي الْأَرْضِ كَانَ مَنْ شَهِدَهَا فَكَرِهَهَا كَانَ كَمَنْ غَابَ عَنْهَا، وَمَنْ غَابَ عَنْهَا فَرَضِيَهَا كَانَ كَمَنْ شَهِدَهَا»**

**"Dhambi linapotendeka katika ardhi, anayeliona na kulikataa atachukuliwa kama mtu ambaye hakuwepo, lakini asiyekuwepo na akaliidhinisha atakuwa kama yule aliyeiona."** Na katika riwaya ya Muslim:

**«إِنَّه يُسْتَعْمَلُ علَيْكُم أُمَراءُ، فَتَعْرِفُونَ وتُنْكِرُونَ، فمَن كَرِهَ فقَدْ بَرِئَ، ومَن أنْكَرَ فقَدْ سَلِمَ، ولَكِنْ مَن رَضِيَ وتابَعَ»**

**"Mtakuwa na watawala baadhi yao mnaowaridhia na baadhi yao mtawakataa. Asiyewapenda atasalimika, na atakayekanusha atasalimika, lakini anayeridhia na kuwafuata (hakika atakuwa ni mwenye dhambi)".**

Yaani, mwenye kuridhishwa na kufuata, bila ya kuchukia wala kukataa ndiye atahisabiwa na kuadhibiwa.

Msiruhusu wingi wa waovu utikisike au kukufanyeni kusitasita. Mwenyezi Mungu Mtukufu asema:

**[قُل لَّا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيثِ فَاتَّقُوا اللهَ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ]**

**“Sema: Haviwi sawa viovu na vyema ujapo kupendeza wingi wa viovu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili, ili mpate kufanikiwa.”**[Surat Al-Ma’idah:100].

Yaani, wenye kuasi na watiifu hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu, hata kama idadi ya wakosefu ni kubwa na idadi yao ikakuvutieni kwa sababu wale wanaomtii Mwenyezi Mungu ndio wenye kufaulu watapata malipo yake Siku ya Kiyama hata wakiwa wachache. Ama wenye kuasi hao ndio wenye hasara hata wakiwa wengi. Basi muonyesheni Mwenyezi Mungu yale Anayoyapenda na Anayoridhika nayo: misimamo iliyo wazi, ya kijasiri na isiyo na utata.

**[فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ وَأَنتُمُ الْأَعْلَوْنَ وَاللَّهُ مَعَكُمْ وَلَن يَتِرَكُمْ أَعْمَالَكُمْ]**

**“Basi msiregee na kutaka suluhu, maana nyinyi ndio mtakao shinda. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja nanyi, wala hatakunyimeni malipo ya vitendo vyenu.”** [Surat Muhammad:35].

**H.** 4 Dhu al-Hijjah 1446
**M. :** Jumamosi, 31 Mei 2025

**Hizb ut Tahrir**
**Wilayah Lebanon**